

madhehebu yale yaliyokuwa safi na yamekuwa maasi sasa kwa kuwa ujumbe huu unafuata onyo la hukumu, lazima utolewe siku za mwisho, kwa hivyo haiwezi kuwa ni kanisa la Kirumi, kwa kuwa kanisa hilo lilikuwa limeanguka karne nyingi zilizopita. Zaidi ya hayo, katika sura ya 18 ya ujumbe ambao ni wa wakati ujao, watu wa Mungu waitwa kutoka kwake Babeli". Vita kuu uk.383.

"Kwa Babeli wa nyakati hizi imesemwa, "dhambi zake zimefika hata mbinguni na Mungu amekumbuka maovu yake." (Ufunuo 18 :5) Amekijaza kikombe cha machukizo yake na uaribifu unamkaribia. Lakini Mungu ana watu humo Babeli ;na kabla ya hukumu zake, hao waaminifu lazima waitwe kutoka humo, ili kwamba "wisishiriki dhambi zake, wala kuyapokea mapigo yake." Kuanzia hapo, mshindo mkuu huo unaolinganishwa na malaika arukaye kutoka mbinguni, akiuangazia ulimwengu kwa utukufu wake, na kulia kwa nguvu na kuweka wazi dhambi za Babeli, pamoja na ujumbe wake, wito unatolewa "Tokeni kwani enyi watu wangu". Ujumbe huu wake ukiambatana na ujumbe wa Malaika watatu, utafikia kuwa kilio kikuu

"Roho ya unabii gombo la nne 422.

"Dhambi za babeli zitawekwa wazi. Matukio ya kutisha ya kuungana kwa kanisa na serikali, matayalisho ya umisimu, mbinu za uongo zinazokuja haraka za Rumi... yote yatawekwa wazi. Kupitia kwa maonyo hayo ya kutisha, watu wataamshwa. Maelfu na maelfu hawajawahi kusikia maneno kama haya. Kwa mshangao mkuu wanasikia ushuhuda kuwa Babeli ni kanisa, lililoanguka kwa makosa na dhambi, sababu ya kukataa kwake ukweli aliotumiwa kutoka mbinguni.

Watu watawaendea walimu wao wa hapo awali wakitaka kujua mambo hayo ni kweli? Wahubira wanawapa hadithi za kuwandanganya, wanawatabilia mambo laini, ili kutuliza uoga wao, na dha-

miri zao zilizoamka. Bali wengi watakataa kutosheka na uongozi wa watawala hawa, na kuuliza "yameandikwa wapi. "Wahubiri hawa, kama mafarisayo wa zamani, wanajawa na chuki kwa kuona mamlaka yao yanatiliwa shaka ;wanashutumu kama vile shetani, na kuwachochea wengi wa wpenda dhambi

wanajawa na chuki kwa kuona mamlaka yao yanatiliwa shaka ;wanashutumu kama vile shetani, na kuwachochea wengi wa wpenda dhambi kuwatakana na kuwauthi wautangazao .

"Roho ya unabii gombo la nne 424.

"Msukosuko huu unapoingia, watu wengi walio kuwa na mfano wa utaua katika ujumbe wa malaika wa tatu, wala hawakuwa wametakazwa nao, wataacha mahali pao na kukimbilia chini ya pendela la mkuu wa giza. Kwa kuungana na walimwengu na kupokea roho yao, wakaanza kuyatazama mambo na kuamua kama wao , na wakati kujaribiwa kujapo, wako tayari kuchagua njia iliyo rahisi na yenye watu wengi. Watu walio na talanta na wenye kufutia, waliokuwa wakifurahia ukweli hapo awali, watatumia nguvu zao kundanganya na kupotosha roho. Wanakuwa maadui wa kwanza wa ndugu zao. Wakati wa sabato wanaletwa mbele za mahakama ili kujibu maswali juu ya imani yao, hawa waasi ndio wa kwanza kutumiwa na shetani kama mawakala wake kueleza vibaya na kuwahukumu na kwa ripoti za uongo, watapendekeza kwa chuki wakuu kughadhabika juu yao.

"Roho ya unabii gombo la nne uk.426.

Hivyo tunaona kwa wazi kuwa Babeli wa tatu ni kanisa ambalo linadai imani katika ujumbe wa malaika wa tatu lakini halikutakaswa kwa kuamini.



## Je kuna saidi ya Babeli moja?

**Jibu:** Ufunuo 16:19 "Na mji ule mkuu ukagawanyika mafungu matatu, na miji ya mataifa ikaanguka; na Babeli ule mkuu ukakumbukwa mbele za Mungu. Kupewa kikombe cha mvinyo ya ghadhabu ya hasira yake".

Swali: Je neno Babeli linasimamia nini kiroho?

Jibu: Linasimamia mnara wa Babeli (Babloni) Genesis 11:9 "Kwa sababu hiyo jina lake likaitwa Babeli; maana hapo ndipo Bwana alipoichafua lugha ya dunia yote; na kutoka huko Bwana akawatawanya waende usoni pa nchi yote." Maana ya kando ya neno hili ni "Mchafuko".

Swali: Kanisa la Mungu limefafanuliwa aje na maadiko?

Jibu : Jeremiah 6 :2 "Binti sayuni aliye mzuri, mwororo" Jeremiah 3 :14 "Rudini, enyi watoto wenye kausi, asema Bwana ; maana mimi ni mume wenu"

Jeremiah 31 :32 "Si kwa mfano wa agano lile nililolifanya na baba zao, katika siku ile nilipowashika mkono, ili kuwatoa katika nchi ya Misri ; ambalo agano langu hilo walilivunja, ingawa nalikawa mume kwao, asema Bwana".

2 Wakorintho 11 :2 "Maana nawaonea wivu,

wivu wa Mungu ; kwa kuwa naliwaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi".

Swali :Je Mungu alionaje kanisa lake linalompa kisogo, likienda kinyume cha neno lake na ushauri

◆ This is a go ye out to meet him publication ◆

Testimony Press Publications  
PO Box 286 Tonasket WA 98855 USA  
www.testimonypress.com

na kuingia katika uasi ?

Jibu : Yakobo 4 :4 ``Enyi wazinzi, hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu ? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu.’’

Isaya 1 :21 ``Mji huu uliokuwa mwaminifu umeku-waje kahaba ! yeye aliyejaa hukumu ya haki ; haki ilikaa ndani yake, bali sasa wauaji’’.

Swali : Mungu anaiitaje Babeli ?

Jibu :Ufunuo 17 :4,5 ``Na mwanamke yule alikuwa amefikwa nguo ya rangi ya zambarau na nyekundu, amepambwa kwa dhahabu, na kito cha dhamani, na lulu, naye alikuwa na kikombe cha dhahabu mkononi mwake, kilichojawa na machukizo, na machafu ya uasherati wake. Na katika kipaji cha uso wake alikuwa na jina limeandikwa, la siri Babeli mkuu mama wa makahaba na machukizo ya inchi.

### **Babeli wa kwanza**

Swali : Ufunuo 16 :19 Inatuonyesha kwamba Babeli iligawanyika mafungu matatu, je tutajuaje mafungu haya matatu ?

Jibu :Fungu la kwanza la Babeli ni Rumi inayoelezwa katika Ufunuo 17 :4-6. Ndiyo iliyokuwa Kanisa la kwanza kuanguka na kujiunga na serikali pamoja na kuteza watakatifu. Kwa hivyo neno linamshuhudia kuwa mama wa makahaba.Ufunuo 17 :6 ``Nikamwona yule mwanamke amelewa kwa damu ya watakatifu, na kwa damu ya mashahidi wa Yesu, nami nilipomwona nikastaajabu ajabu kuu’’.

``Katika karne ya kumi na tatu ndipo palipoanzishwa ukatili na uovu mkuu wa upapa. Mkuu wa giza

alitawala pamoja na watawala wa kanisa la Kirumi katika mikutano yao mikuu ya siri, shetani na malaika zake waliongoza, huku malaika wa Bwana bila kuonekana akiandika maovu yao, na historia ambayo ni ya kutisha kuwekwa mbele za macho ya kibinadamu.``Babeli aliye mkuu’’ ``alikuwa amelewa kwa damu ya watakatifu’’.

fu’’Mamilioni ya waliouawa kwa sababu ya ukweli wa Mungu, walilia ili awalipizie kwa uongozi huo ulioasi. Nuru ya mchana ya kipapa ndiyo iliyokuwa giza kuu la ndunia’’. Roho ya unabii gombo la nne 63,64.

``Kwenye ufunuo 17, Babeli amefananishwa na mwanamke, na limetumiwa katika maandiko kuamaanisha kanisa. Mwanamke mwema akifanana na kanisa safi na mwanamke mbaya akifanana na kanisa lililo asi.Babeli anatabulikana kuwa kahaba ; na nabii aliona akiwa amelewa kwa damu ya watakatifu. Huyu Babeli basi amesimamia Rumi, kanisa lililoasi na kuwaua wafuasi wa Kristo’’ Roho ya unabii gombo la 4,233

### **Babeli wa pili ;**

Kabla hatujasoma Babeli wa pili ni ipi, lazima tujue kuwa itakuwa imeungana na Babeli wa kwanza na kuwa na mafundisho kama ya yule wa kwanza.

Swali : Je Babeli wa pili ni nani ?

Jibu : Babeli wa pili ako mbali sana na wa kwanza katika ufunuo 17 ; na nabii ametupa jibu katika Roho ya unabii gombo la nne uk.232 ; ``Wakati makanisa yalidharau mashauri ya Mungu kwa kukataa ujumbe wa marejeo ya Yesu,Bwana aliwakataa .Malaika wa kwanza alifuatwa na wa pili, akitangaza,``umeanguka, umuanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanyweshwa mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake’’.(ufunuo 14 :8) Ujumbe huu, wa kiadventista waliulewa kwamba, lilikuwa anguko la makanisa baada yao kukataa ujumbe wa malaika wa kwanza. Tangazo kwamba ``Babeli imeanguka,’’ lilitangazwa msimu wa jua 1844, na matokeo yake,

watu kama elfu hamsini wakatoka kwenye makanisa haya. Neno Babeli lililotolewa kutoka Babuloni linalomaanisha machafuko, linatumika kwenye maandiko kulenga dini za uongo au zilizoanguka.Lakini ujumbe huu unaotangaza anguko la Babeli lazima ulenge dini zilizokuwa nzuri hapo mwanzo lakini zikaasi baadaye. Na haiwezi kuwa

kanisa la Rumi ndilo linatanjwa hapa ; kwa kuwa kanisa hilo lilikuwa katika hali ya kuasi karne nyingi zilizopita. Lakini linaingiana na makanisa ya kiprotestanti, wote wanadai kutoa misingi ya mafundisho yao kwenye Bibilia, lakini wakiwa wamegawanyika vikundi visivyohesabika. Umoja aliouombea Kristo haupo. Badala ya Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja, kuna maongozi na makisio ya tafsiri ya neno la Mungu mengi yasiyohesabika.Dini saa hizi inaonekana imechanganyikiwa na kutokuwa na mpango hivyo watu wa dunia hii hawajui waamini nini kama ukweli. Mungu hayuko katika hizi zote ; hizi ni kazi za watu, kazi ya shetani,

Roho ya unabii gombo la nne 232.

Tunaona hapa kwamba mtumishi wa Bwana anaeleweka vizuri kwamba Babeli ya ufunuo 14 :8 Si Rumi kabisa, bali waprotestanti wa 1844 waliokataa ujumbe wa malaika wa kwanza wa ufunuo 14. Hawakuwa Babeli hata ujumbe wa wakati huo walipoukataa na kuwaudhi walioufuata ukweli.

### **Babeli wa tatu**

Kabla hatujajifunza ni nani Babeli wa tatu, ni lazima tukumbuke kuwa inaunganika na Babeli wa kwanza na wa pili na iwe na mafunzo kama yao.

Swali :Ni nani Babeli wa tatu ?

Jibu :Roho ya unabii gombo la nne limepeana na kutueleza Babeli aina mbili pamoja katika sura ``ujumbe wa malaika wa pili’’ lakini hajasema kitu kuhusu babeli wa tatu na wa mwisho wa ufunuo 18 katika maandiko yake ya kurasa 187, kwanza anaendelea na kuonyesha Babeli wa mwisho atakuwa anafundisha nini katika sura ``uvuvio wa siku hizi’’.

(Imani pekee ,hakuna bidii inayohitajika). Baadaye anaelezea ukweli kwamba makanisa wanaopenda dunia watakuwa na bidii na juhudi nyingi lakini bila Roho ya Mungu,itaifanya kuwa Babeli wa tatu. Ujumbe huu ungekuwa ni wa wakati ujao.``Ujumbe wa ufunuo 14 unaotangaza anguko la Babeli, lazima ulenge kwenye